JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

## KIKAO CHA AROBAINI NA TISA

**20 JUNI, 2019**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

_______________

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

## KIKAO CHA AROBAINI NA TISA – TAREHE 20 JUNI, 2019

## I. DUA:

## II. MASWALI:

### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**411. MHESHIMIWA ANNA JORAM GIDARYA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Shule za Sekondari za Serikali za Kata zilizopo katika maeneo mengi zinakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa Walimu na Mabweni ya kulala Wanafunzi, jambo ambalo linachangia kufeli kwa Wanafunzi wa kike kutokana na mazingira hatarishi kwa elimu na afya ya mtoto wa kike:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga Bweni kwa kila Shule ya Kata ili kuwaondolea Watoto kero za kutembea umbali mrefu kwa miguu;

(b) Je, Serikali ina mikakati na mipango gani kwa Shule ambazo Wanafunzi wake wamepanga

vyumba mitaani kwa kuwa mazingira hiyo siyo rafiki kwa Watoto wetu wa kike.

**412. MHESHIMIWA DESDERIUS JOHN MIPATA (NKASI KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Ujenzi wa barabara ya Namanyere – Ninde yenye urefu wa kilomita 67 bado haujakamilika licha ya madaraja na makalvati yote kujengwa na kuwa tayari:-

(a) Je, ni lini barabara hiyo itakamilika na kurudisha mawasiliano kwa Wananchi wa Kata ya Ninde;

(b) Daraja linalounganisha Kijiji cha Ninde na Namansi lilikatika na kukata mawasiliano baina ya Vijiji hivyo na taarifa ilikwishafikishwa TARURA; Je, ni lini ujenzi wa daraja hilo utaanza.

## OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

**413. MHESHIMIWA FREDY ATUPELE MWAKIBETE (BUSEKELO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, ni lini Serikali itaanza kutumia mifumo ya *Open Source Software* kwenye Taasisi na Idara za Serikali.

**414. MHESHIMIWA FAKHARIA SHOMAR KHAMIS (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):- Zanzibar kuna mradi wa TASAF ambao unafanya kazi nzuri na hayo ndiyo matunda ya Serikali ya Muungano:-

(a) Je, tangu kupelekwa kwa mradi wa TASAF Zanzibar ni miradi mingapi mingine na ya aina gani ambayo imepelekwa Zanzibar;

(b) Je, mradi wa TASAF umegharimu fedha kiasi gani ambayo imewanufaisha Wananchi kwa kuwapunguzia umaskini.

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

**415. MHESHIMIWA LUCIA MICHAEL MLOWE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:- Serikali imekuwa ikitoa ahadi juu ya uanzishwaji wa mradi wa Mchuchuma na Liganga na Wananchi wana shauku sana na mradi huu:-

Je, ni lini sasa mradi huu utaanza.

**416. MHESHIMIWA ZUBERI MOHAMED KUCHAUKA (LIWALE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:- Kumekuwa na tatizo la muda mrefu la ukosefu wa soko kwa mazao ya jamii ya kunde kama mbaazi na choroko:-

(a) Je, ni nini kauli ya Serikali juu ya kutatua tatizo hilo;

(b) Je, ni nini mkakati wa Serikali juu ya kuongeza thamani kwa mazao hayo ili kuimarisha masoko ya mazao hayo.

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

**417. MHESHIMIWA MUSSA BAKARI MBAROUK (TANGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Kwa muda mrefu hakuna usafiri wa uhakika kati ya Pemba na Tanga hali inayopelekea vyombo vya usafiri vya kienyeji kupata ajali mara kwa mara na kupoteza maisha ya watu na mali zao:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kununua meli ya kisasa na ya uhakika ili kuokoa usafiri wa Tanga – Pemba.

**418. MHESHIMIWA VENANCE METHUSALAH MWAMOTO (KILOLO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:-

Je, ni adhabu gani anastahili kupewa Mkandarasi anaposhidhwa kumaliza mradi wowote kwenye Halmashauri kwa wakati.

**419. MHESHIMIWA JUMA KOMBO HAMAD (WINGWI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Barabara ya Dar es Salaam – Morogoro – Dodoma ni muhimu sana kwani inaunganisha Jiji la kibiashara la Dar es Salaam na Makao Makuu ya Nchi Dodoma; hata hivyo barabara hii ina changamoto nyingi sana ikiwemo kuwa na mashimo pamoja na kuwa nyembamba:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati mashimo hayo pamoja na kuipanua barabara hiyo.

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

**WIZARA YA KILIMO:**

**420. MHESHIMIWA QAMBALO WILLY QULWI (KARATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:- Wakulima wa Bonde la Eyasi Kilimo chao ni cha Umwagiliaji kwa kutumia chanzo cha Chemchem za Qangded. Kutokana na kupungua kwa kiasi cha maji katika vyanzo hivyo, Wakulima wengi wameshindwa kuzalisha:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza vyanzo mbadala kama Mabwawa na Visima virefu ili kilimo katika Bonde hili kiwe endelevu.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Kwamba, Bunge likubali kujadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Kwamba, Bunge likubali kupitisha Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

***(Majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA** **S. KAGAIGAI**
**20 JUNI, 2019** **KATIBU WA BUNGE**